

TANZANIA

Registered this.....5th  
day of August 2020  
Asst. Registrar of Cooperative Societies



**UDOM SACCOS**  
*Pamoja Tujenge Uchumi Wetu*

## **CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO CHUO KIKUU CHA DODOMA**

(UDOM SACCOS LTD)  
NA. YA USAJILI: DOR 715

## **SERA YA UFUATILIAJI MADENI**

Imetengenezwa Chini ya Kanuni ya 5(3)(c) ya Huduma Ndogo za Fedha (SACCOS) 2019

Imeandaliwa na Bodi ya UDOM SACCOS LTD  
S.L. P 2765

Barua Pepe: [udomsaccosltd@gmail.com](mailto:udomsaccosltd@gmail.com)  
DODOMA- TANZANIA

**Toleo I: 2020**

## YALIYOMO

|  |    |
|--|----|
| 1.1 Utangulizi .....   | 2  |
| 1.2 Statementi ya Sera .....   | 2  |
| 1.3 Maregeo ya Sheria Mbalimbali .....                                       | 2  |
| 1.4 Walengwa wa Sera Hii .....   | 3  |
| 1.5 Wamiliki wa Sera Hii .....   | 3  |
| 1.6 Mambo yanayoweza kupelekea Mkopo kushindwa kurejeshwa kwa wakati .....   | 3  |
| 1.7 Athari za Mkopo Kuchelewa Kurejeshwa.....                                | 4  |
| 1.8 Taarifa za Mikopo kwa Umri .....   | 5  |
| 1.9 Ufutiliaji wa Marejesho ya Mkopo .....                                   | 7  |
| 1.10 Taratibu za Kufutililia Madeni Kwenye kila Kundu la Umri wa Mikopo..... | 7  |
| 1.11 Ukamataji wa Dhamana.....   | 8  |
| 1.12 Taratibu za Akiba kulipa Mkopo na Uuzaji wa Dhamana Nyinginezo.....     | 8  |
| 1.13 Gharama za Ufutiliaji Madeni .....                                      | 9  |
| 1.14 Matumizi ya Dalali .....  | 9  |
| 1.15 Mgawangyo wa Fedha za Mauzo ya Dhamana.....                             | 10 |
| 1.16 Haki Juu ya Dhamana.....  | 10 |
| 1.17 Kutumia Mahakama .....  | 11 |
| 1.18 Pembetatu ya Ufutiliaji Madeni.....                                     | 11 |
| 1.19 Ufutaji Mikopo Vitabuni .....   | 12 |
| 1.20 Ufutiliaji Mkopo Baada Ya Kusutwa Vitabuni.....                         | 13 |
| 1.21 Uhuishaji wa Sera.....  | 13 |
| 1.22 Uidhinishwaji wa Sera.....  | 14 |

## **1.1 Utangulizi**

UDOM SACCOS Ltd ni Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo kilichosajiriwa kwa nambari ya usajilil DOR 715 mnamo tarehe 05 Januari 2011 chini ya Sheria ya Vyama vya Ushirika na. 20 ya mwaka 2003 kama ilivyofutwa na kuendelea kutambulika kwa yote yaliofanywa chini ya Sheria hiyo na Kifungu cha 144(2) cha Sheria ya Vyama vya Ushirika nambari 6 ya mwaka 2013. Mfungamano wa UDOM SACCOS Ltd umegawanyika katika makundi saba kama ifuatavyo;:-

- (i) Wafanyakazi wa Chuo Kikuu cha Dodoma
- (ii) Watendaji wa UDOMA SACCOS Ltd
- (iii) Waliokua Wafanyakazi wa Chuo Kikuu cha Dodoma na kuhamia Taasisi na Mamlaka nyingine za Serikali

## **1.2 Statementi ya Sera**

Biashara ya ukopeshaji ni ya imani kwamba mkopo utarejeshwa kwa mujibu wa makubaliano ndani ya mkataba wa mkopo, lakini kuna sababu mbalimbali zinazoweza kupelekea mkopo huo usirejeshwe kwa wakati kama vile sababu za kitaasisi, sababu za mkopaji na sababu za mazingira zilizo nje ya taasisi na mkopaji.

Kwa hali hii, utaratibu maalum unahitajika ili kuhakikisha mikopo japo inaweza kuchelewa lakini inarejeshwa. Kwa upande mwingine Sera hii ni utekelezaji wa mahitaji ya Sheria ya Ushirika, 2020 na Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Na. 10 ya Mwaka 2018 na hususani Kanuni ya 79 za Huduma Ndogo za Fedha (SACCOS) za Mwaka 2019.

## **1.3 Marejeo ya Sheria Mbalimbali**

Sera hii imetengenezwa kwa kuzingatia sheria mbalimbali za Nchi ikiwemo:-

- (i) Misingi Saba (7) ya Ushirika 1995
- (ii) Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania 2002
- (iii) Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha (Microfinance) 2017
- (iv) Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013
- (v) Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Na. 10 ya mwaka 2018
- (vi) Sheria ya Kodi ya Mapato ya 2004
- (vii) Sheria ya Utawala wa Kodi, 2015

- (viii) Sheria ya Usimamizi wa Mifuko ya Hisadhi ya Jamii, 2018
- (ix) Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya 2006
- (x) Viwango vya Kimataifa vya utoaji Taarifa (IFRS)
- (xi) Kanuni za Jumla za SACCOS 2019
- (xii) Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha (SACCOS) 2019
- (xiii) Kanuni za Vyama vya Ushirika 2015
- (xiv) Masharti ya UDOM SACCOS Ltd

#### **1.4 Walengwa wa Sera Hii**

Walengwa wa sera hii kama wafuatao:-

- (1) Wanachama
- (2) Viongozi wa Bodi na Kamati ya Usimamizi
- (3) Kamati ya Mikopo
- (4) Watendaji
- (5) Wasimamizi wa Sheria kama vile Benki Kuu na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania
- (6) Waajiri katika Taasisi walipo Wanachama
- (7) Wadau wengineo (Wakusanya Madeni, Wakaguzi, Wakopeshaji wa Nje, Washauri, n.k)

#### **1.5 Wamiliki wa Sera Hii**

Japo sera hii imetengenezwa na Bodi na Kuidhinishwa na Mkutano Mkuu, Wasimamizi Wakuu wa utekelezaji wa sera hii ni Kamati ya Mikopo.

#### **1.6 Mambo yanayoweza kupelekwa Mkopo kushindwa kurejeshwa kwa wakati**

- (i) Sera ya Mikopo kupitwa na wakati
- (ii) Utoaji wa mikopo kwa kutozingatia matakwa ya Sera ya Mikopo
- (iii) Mikopo kutokua na dhamana
- (iv) Viongozi Waandamizi Kamati Mwenyekiti na Makamu wake kuingilia/kushawishi ama kutumia nguvu ya mamlaka yao kushinikiza utolewaji wa mikopo kwa baadhi ya Wanachama ambao sifa zao zimepungua
- (v) Kutowanisha muda wa mkopo na muda wa mkataba wa ajira

- (vi) Kutofanya upembuzi wa kutosha wa mkopo juu ya uwezo wa kurejesha kutokana na mapato ya sasa na ya baadaye pamoja na hadhi na uhalali wa dhamana
- (vii) Kutosajili dhamana
- (viii) Mwajiri kuchelewesha makato
- (ix) Kuacha na kupunguzwa kazi kwa Wanachama kwenye ajira zao za msingi
- (x) Kutoa mkopo mkubwa ama mdogo tosauti na malengo ya mkopaji
- (xi) Sababu za mkopaji na kutotoa ushirikiano
- (xii) Woga wa viongozi kuanzisha mchakato wa kufuutilia madeni kwa nguvu moja

### **1.7 Athari za Mkopo Kuchelewa Kurejeshwa**

- i) Kupungua kwa ukwasi (liquidity)
- ii) Kupungua kwa kasi ya utoaji mikopo
- iii) Kuchelewa kupata mapato
- iv) Kuongezeka kwa malalamiko ya Wanachama
- v) Kuchafua taarifa za mikopo
- vi) Kamati ya Usimamizi inaweza kusimamizi utoaji mikopo mipyä endapo mikopo iliyoko kwenye hatari (Portfolio At Risk – PAR) zaidi ya siku 30 ni 10% na zaidi
- vii) Kupungua kwa mapato kunaweza kupunguza faida ama kusababisha Chama kupata hasara
- viii) Ufutaji wa mikopo unaongezeka
- ix) Matengo ya mikopo mibaya yanayotokana na umri wa mikopo huongezeka
- x) Kupungua kwa Matengo ya mikopo mibaya yanayotokana na 15% ya faida
- xi) Kushuka kwa mtaji wa Chama
- xii) Wasimamizi wa Sheria – Benki Kuu inawenza kufanya ukaguzi na kutoa maclekezo magumu, na endapo hali ya mikopo mibaya inacndelea inaweza kupelkeea kufutiwa leseni

## 1.8 Taarifa za Mikopo kwa Umri

| KUNDI                                    | UMRI<br>SIKU | KIASI CHA<br>MKOPO | TENGO LA MIKOPO<br>MIBAYA |     |
|--|--------------|--------------------|---------------------------|-----|
|  |              | TZS                | %                         | TZS |
| Ndani ya kiwango (Current)               | 0 - 30       |                    | -                         |     |
| Angalizo (Watch/Especially<br>Mentioned) | 31 - 90      |                    | 10%                       |     |
| Chini ya Kiwango (Substandard)           | 91 - 180     |                    | 30%                       |     |
| Mashaka (Doubtful Debts)                 | 181 - 365    |                    | 50%                       |     |
| Hasara (Loss)                            | 365+         |                    | 100%                      |     |

Sera ya ufuatiliaji madeni inaanza kufanya kazi katika kundi la angalizo hadi hasara.

Taarifa ya mikopo inayoandaliwa kila robo mwaka kwa ajili ya Kamati ya Mikopo na Bodi itakuwa na schemu kuu nne (4) kama ifuatavyo;

- i) Taarifa za jumla za Chama
- ii) Taarifa ya Umri wa Mikopo
- iii) Taarifa ya Tengo la Madeni mabaya
- iv) Ubora wa Mikopo

Jedwali lifuatalo linaonesha muundo wa taarifa ya mikopo:

# UDOM SACCOS LTD

## TAARIFA YA MIKOPO KAMA TAREHE ..... 20.....

|   |  |            |
|---|--|------------|
| 1 | Mikopo na Viasharia Mbalimbali vya Ufanisi wa Mikopo                 | .....20... |
|   | Idadi ya Wanachama waliopo (Mwisho wa Kipindi)                       |            |
|   | Thamani ya Mikopo iliyotolewa (Ndani ya Kipindi)                     |            |
|   | Idadi ya Mikopo iliyotolewa (Ndani ya Kipindi)                       |            |
|   | Thamani ya Mikopo kwa Wanachama (Mwisho wa Kipindi)                  |            |
|   | Idadi ya Mikopo ya Wanachama (Mwisho wa Kipindi)                     |            |
|   | Wastani wa Mikopo kwa Wanachama (Mwisho wa Kipindi)                  |            |
|   | Thamani ya Marejesho yaliyochelewa (Mwisho wa Kipindi)               |            |
|   | Thamani ya Mikopo iliyochelewa (Mwisho wa Kipindi)                   |            |
|   | Thamani ya mikopo iliyorekebishwa restructured (Mwisho wa Kipindi)   |            |
|   | Thamani ya Mikopo ulioongezewa/re-finance (Mwisho wa Kipindi)        |            |
|   | Thamani ya Mikopo iliyofutwa (Mwisho wa Kipindi)                     |            |
|   | Thamani ya Marejesho Msingi Yaliyotajiwa Kulipwa (Mwisiho wa Kipind) |            |
|   | Thamani ya Marejesho msingi yaliyolipwa (Mwisho wa Kipindi)          |            |
|   | Thamani ya Marejesho msingi yaliyolipwa ndani ya wakati              |            |
|   | Thamani ya Marejesho msingi yaliyolipwa mbele -prepaid               |            |
|   | Wastani wa Kiwango cha Mkopo kwa Mwanachama                          |            |
|   | Wastani wa Muda wa Mkopo   |            |

### Tengo la Mikopo

| Kundi       | Siku             | Idadi ya Mikopo | Rejesho Chelewa (Tsh) | Mkopo Chelewa (Tsh) | PAR | Tengo (%) | Tengo (Tsh) |
|-------------|------------------|-----------------|-----------------------|---------------------|-----|-----------|-------------|
| 2<br>&<br>3 | Kiwango          | 0 - 30          |                       |                     |     |           |             |
|             | Angalizo         | 31 - 90         |                       |                     |     | 10%       |             |
|             | Chini ya Kiwango | 91 - 180        |                       |                     |     | 30%       |             |
|             | Mashaka          | 180 - 365       |                       |                     |     | 50%       |             |
|             | Hasara           | 365+            |                       |                     |     | 100%      |             |
|             | Jumla            |                 |                       |                     |     |           |             |

Jumla ya Thamani ya Mikopo kwa Wanachama (Tsh)

Tengo la Mikopo Mibaya (%)

Urejeshwaji Mikopo (Repayment Rate) (%)

Mikopo iliyoko kwenye hatari zaidi ya siku 30 (PAR) (%)

Mikopo isiyo na Ufanisi zaidi siku 180(NPL) (%)

**Viwango kubalika:** PAR  $\leq$ 5% , NPL  $\leq$ 2%, Urejeshaji Mikopo  $\geq$ 95%

### **1.9 Ufutiliaji wa Marejesho ya Mkopo**

- (a) Kila mwanachama ana wajibu kuhakikisha kuwa marejesho ya mikopo aliyochukua yanafanyika kama ilivyokubaliwa.
- (b) Afisa Mikopo atahusika mara kwa mara kutengenenza taarifa ya hali halisi ya mikopo kila mwezi na kuwakumbusha Wanachama kulipa mikopo yao kwa wakati
- (c) Afisa Mikopo ataishauri Kamati ya Mikopo na Bod kupitia Meneja hali ya mikopo mibaya na hatua za kuchukua kisheria na kitalaam

### **1.10 Taratibu za Kufutililia Madeni Kwenye kila Kundu la Umri wa Mikopo**

Chama kitachukulia Mwanachama ameshindwa kurejesha mkopo wake wote endapo schemu ya mkopo au sehemu ya rejesho la msingi ama schemu ya rejesho la riba limeshindwa kukamilika na kuja kwa wakati ama kuchelewa kwa muda wa siku zaidi ya 30.

Hivyo, taratibu zifuatazo zitafuatwa kufutililia madeni:-

- i) Mkopo uliochelewa siku 1-30: Mwanachama atakumbushwa kwa simu na wadhamini wake juu ya kuheshimu mkataba wa mkopo kwa kufanya marejesho yake yanayochelewa. Kila wiki ndani ya siku 30 kukumbushwa kwa simu kutafanywa na Afisa Mikopo. Taarifa ya ufutiliaji katika hatua hii itaandaliwa na Afisa Mikopo
- ii) Mkopo ukiendelea kuchelewa zaidi ya siku 30: Barua za kumkumbusha Mwanachama na Wadhamini zitaanza kutolewa kama ifuatavyo:
  1. Barua ya kwanza (demand note) na nakala kwa mkopaji na wadhamini wake ikiwa ni taarifa na kupewa muda wa siku 14 awe amefanya marejesho yake.
  2. Kama ndani ya muda siku 14 za awali hakuna kilichofanyika barua ya pili (demand note) kwa mkopaji na nakala kwa wadhamini itatolewa kwa kupewa muda wa siku 14 tena kuwa wamefanya marejesho.

3. Kama ndani ya siku 14 za pili hakuna mwitikio wowote kutoka kwa Mwanachama au Wadhamini wake, barua ya tatu kwa mkopaji na nakala kwa Wadhamini ikionesha kupewa siku 14 nyingine na endapo atashindwa kusanya marejesho yake hatua za kisheria zitafuata ikiwa ni pamoja na kuanza mchakato wa kutumia na kuuza dhamana kulipia mkopo.
4. Kama ndani ya siku 14 kwa mara ya tatu hakuna kilichofanyika, barua ya kisheria itaandikwa kumtaarifu mkopaji na wadhamini kuanza kwa zoezi la kutumia na kuuza dhamana zao (wote Mkopaji na Wadhamini) kulipia mkopo. Chama kitaanza kuuza dhamana za mdhamini na endapo hazitoshelezi kulipa deni la mkopo wote, Chama kitaendelea na dhamana za wadhamini.
5. Hatua za kuchukua akiba za mkopaji na wadhamini kulipia mkopo zitaanza, kama bado mkopo haujalipwa kwa ukamilifu, zoezo la kuuza mali nyingine zilizowekwa kama dhamana litafuata cndapo akiba hazitatosheleza.

## 1.11 **Ukamataji wa Dhamana**

- (1) Baada ya notisi za siku 14 mara tatu, Chama kitafanya jitihada za kukamata mali za magari, mitambo na mashine ili ziwekwe chini ya uangalizi wake kwa ajili ya kusubili taratibu za uuzaaji.
- (2) Kwa dhamana za ardhi na majengo, taratibu katika aya ya 1.12(2)(ii) na (3) za sera hii zitatumika

## 1.12 **Taratibu za Akiba kulipa Mkopo na Uuzaji wa Dhamana Nyinginezo**

(1) Kutokana na Mkataba wa Mkopo, Chama kitakuwa na Mamlaka ya kutumia dhamana ya Hisa za Hiari, Akiba au Amana za Mkopaji na Wadhamani kulipia mkopo mara baada ya kutoa notisi mara tatu pamoja na notisi ya mwisho ya siku 14 kumtaarifu Mwanachama kwamba Chama kitatumia Hisa za Hiari, Akiba au Amana zilizowekwa kama dhamana ya mkopo kulipia mkopo

(2) Kwa wakati mmoja Chama kina haki ya kutumia dhamana za Wadhamni (hisa za hiari, akiba au amana) kulipia mkopo kutokana na mawasiliano yote aliyokuwa akipata mkopoaji (notisi)

Wadhamini wake walikua wanapata nakala, hivyo, notisi husika inatolewa kwa kulenga kutoa taarifa pande zote za mkopaji na wadhamini.

(3) Kwa dhamana za mali taratibu zitakuwa kama ifuatavyo;

i. Kwa Dhamana za Magari, Mitambo na Mashine Chama kitatoa notisi ya ziada ya siku 30 kumtaarifu Mwanachama na Wadhamini wake kwamba Chama kitaiza mali hizo ili kulipia mkopo

ii. Kwa Dhamana za Ardhi na Majengo: Chama kitafanya tathmini ya thamani (valuation) ya dhamani ya sasa, baada ya tathmini ya thamani Chama kitatoa notisi ya ziada ya siku 60 kumtaarifu Mwanachama na Wadhamini wake kwamba Chama kitaiza mali hizo ili kulipia mkopo

(4) Kama dhamana ya ardhi na majengo itakuwa haijasajiriwa (equitable mortgage), Chama kitafungua shauri Mahakamani ili kuomba kibali cha kuuza mali hiyo baada ya notisi ya ziada ya siku 60 kuisha. Endapo kama dhamana ya ardhi na majengo itakuwa imesajiriwa kwa Msajiri wa Hati (legal mortgage), basi Chama kitakua na haki moja kwa moja ya kuuza bila kuomba kibali cha Mahakama baada ya notisi ya ziada ya siku 60 kuisha.

### **1.13 Gharama za Ufutiliaji Madeni**

Gharama zote za ufutiliaji madeni ambazo Chama kitaingia, zitaongezwa kwenye mkopo na kulipwa na Mkopaji kwa ujumla wake kama sehemu ya mkopo.

### **1.14 Matumizi ya Dalali**

(1) Chama kinaweza kutumia Wakusanya madeni (Madalali) waliotambuliwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania inapoona hatua za ndani hazitoi uhakika wa mkopo kurejeshwa. Ikifika wakati wa kutumia Dalali Chama kitatoa tangazo la zabuni kwa makampuni au taasisi zilizothibitishwa na Mrjis na kupewa kibali ndizo zitaruhusiwa kuomba na upembuzi utafanyika kwa mfumo wa zabuni kumpata mshindi kama ilivyoelekezwa kwenye Sera ya Uhasibu na Fedha ya Chama.

(2) Chama kinaweza kutumia Madalali katika zoezi la ukamataji wa mali za Magari, Mitambo na Mashine kabla ya kuziuza ili ziwe chini ya uangalizi wa Chama

(3) Gharama za Dalali zitalipwa na Chama kwa mfumo wa asilimia (%) iliyokubaliwa katika mkataba kutokana na makusanyo ya marcjesho kutoka kwa mdaiwa.

(4) Mazingira yanayoweza kupelekwa Chama kutumia Dalali:

i) Kama uwezo wa ndani ya Chama kufuatilia mkopo utathibitika kuhitaji dalali anaweza kuongeza nguvu katika zoezi husika.

ii) Kwa amri ya Mahakama ama Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania.

iii) Kama Mwanachama ametoweka na Chama hakina namna yoyote ile ya kumpata

(5) Mkataba kati ya Chama na Dalali husika lazima uidhinishwe na Mrajis Msaidizi wa Mkoa.

(6) Ni MUIIIMU sana kwa Chama kuwa na mkataba maalum wa viwango vya huduma ili kuhakikisha dalali anafikia malengo yaliyokusudiwa na Chama katika kukusanya madeni. Pamoja na mambo mengine, mkataba huu utaclezza haki, wajibu na majukumu ya kila pande ikiwemo fidia endapo malengo hayatafikia.

#### **1.15 Mgawanyo wa Fedha za Mauzo ya Dhamana**

Baada ya dhamana kuuzwa, kodi za Serikali zitalipwa kwa viwango vya wakati huo, mkopo, riba, adhabu na gharama nyinginzo za usuatiliaji madeni zitalipwa na kama fedha itaendelea kubaki, atarcjeshewa Mkopaji.

#### **1.16 Haki Juu ya Dhamana**


(i) UDOM SACCOS Ltd ina haki juu ya dhamana yoyote iliyowekwa na mkopaji na wadhamini wake. Hivyo, Chama kitaamua ni dhamana ipi (kati ya zile za mkopaji na wadhamini) inaweza kuwa ya kwanza kutumika kufidia mkopo kulingana na wepesi, changamoto mbalimbali na gharama zinazohusiana na zoezi la kutumia dhamana kulipia mkopo.

- (ii) Kutokana na Chama kuchukua dhamana kuu na dhamana mbadala, endapo alibaki ya mkopo ni ndogo, Chama kinawenza kuamua kutumia dhamana ndogo mbadala na kuacha dhama kuu (kubwa).

### 1.17 Kutumia Mahakama

Chama kinaweza kufungua kesi Mahakamani kupitia Wanasheria wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania kama kuna tatizo ama mgogoro wowote kwenye dhamana ama Mwanachama mkopaji amekimbia bila kujulikana alipo. Chama kitafungua kesi ili kupata hati ya mahakama ya kukamata mali zozote za mkopaji zilizotambuliwa na kuuzwa ili kufidia mkopo.

### 1.18 Pembetatu ya Ufuatiliaji Madeni



**HATUA YA 1:** Hatua ya kwanza kabisa katika taratibu za usuatiliaji madeni ni kuzungumza (negotiation) ili kujua kwa undani tatizo la mkopaji na kama anaweka ahadi kimaandishi ya kuanza ama kuendelea kusanya marejesho yake hata kama ni kwa kiasi kidogo. Njia hii haina gharama kwa Chama na inajenga mahusiano mazuri kati ya Chama kama Taasisi na Mwanachama. Pia njia hii inawenza kupelekeza kusanya kwa markebishesho (restructuring) ya mkopo ili kuongeza muda kwa lengo la kupungza rejesho kufikia kiasi ambacho Mkopaji anaweza kulipa.

**HATUA YA 2:** Endapo hatua ya kwanza haijafanya kazi mathalani Mkopaji anatoa ahadi na hatimizi ama hatoi ushirikiano wowote, ama hapatikani kwa ajili ya mazungumzo, hatua ya pili

ya kutumia dhamana inaweza kufuata. Dhamana inaweza kutumika kwa misumo mbalimbali kama ifuatavyo; -

- i) Kwa dhamana za hisa za hiari, akiba au amana; Chama kupitia taratibu za kiuhasibu kitatumia dhamana husika kusuta mkopo mara baada ya kutoa notisi kwa mujibu wa aya ya 1.10(ii) ya Sera hii.
- ii) Kama ni dhamana ya mali ya biashara, Chama kinaweza kuweka usimamizi wake ili biashara iendelee na mapato yote yanayopatikana yanaingia kwenye Chama
- iii) Kuiuza kwa taratibu katika aya ya 1.12 za Sera hii.

**HATUA YA 3:** Endapo dhamana haitoshi kulipia mkopo wote ama dhamana ina changamoto mbalimbali ikiwemo kupoteza thamani yake ama kuwa katika mpango mbadala wa Serikali ama migogoro ya kisheria; au Chama hakikuweka dhamana nyingine wakati wa utoaji mkopo; Hatua ya tatu ya kusungua shauri la madai katika Mahakama za Kisheria inaweza kutumika. Angalizo: ni muhimu sana Chama kupata ushauri wa kisheria kabla ya kusungua kesi ya aina hii kutokana na vipingamizi vingi vinavyowezza kujitokeza ikiwemo gharama zisizo tarajiwu.

Chama kama Taasisi kinaweza kuendelea na mchakato wa kusungua kesi Mhakamani ama kutumia Wakili ama kutumia Wanasheria wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika. Bodi itafanya upembuzi wa faida na changamoto za kila njia ili kusikia maamuzi ya busara.

#### 1.19 Ufutaji Mikopo Vitabuni

Kwa mujibu wa taratibu za kiuhasibu na Viwango vya kimataifa vya utoaji taarifa za fedha (IFRS) Mikopo yenye umri wa zaidi ya siku 365 inatakiwa ifutwe katika vitabu vya hesabu. Sifa ya mkopo kusutwa kwenye vitabu vya hesabu ni pale ambapo Chama kimejiridhisha vya kutosha kuwa kwa hatua zilizochukuliwa katika kusuutilia mkopo huo hauwezi kurejeshwa. Sababu zinaweza kuwa uduni wa dhamana, mkopaji na wadhamini ama taratibu mbovu zilizotumika wakati wa kutoa mkopo husika.

Taarifa zitatunzwa kama inavyoilezwa kwenye Kanuni ya 43 za Huduma Ndogo za Fedha (SACCOS) ya Mwaka 2019, hivyo, taratibu za usuataji mkopo ni kama ifuatavyo:

- i) Taarifa ya Meneja kwenda Bodi itaandikwa ikianisha kila mkopo kiasi kilichoidhinishwa, tarehe, marejesho yalisanyika, alibaki ya mkopo siku za kuchelewa, hatua zilizochukuliwa, sababu za kupendekeza kufutwa.
- ii) Bodi watajadili na kusanya maamuzi.
- iii) Baada ya Bodi kufanya maamuzi ya kufuta mikopo husika na muhtasari kuandikwa Mhasibu atafanya zoezi la kufuta mikopo iliyoidhinishwa na Bodi kufutwa kwa kupunguza thamani ya mikopo na kupunguza pia tengo la madeni mabaya kama tengo hilo lina sedha za kutosha kubeba kiasi cha mikopo inayofutwa.
- iv) Kama tengo la madeni mabaya halina sedha za kutosha kufuta mikopo basi kiasi cha mikopo unaofutwa kilichoshindikana kufutwa kupitia tengo la madeni mabaya kitaingizwa kwenye matumizi ya kawaida ya Chama kupitia Kasma ya tengo la madeni mabaya.
- v) Ni vizuri Bodi kuwasiliana na Mrasis Msaidizi wa Mkoa kwa kila hatua kabla na baada ya kufuta mikopo vitabuni. Hii ni kwasababu za kiuwajibikaji kwa Mamlaka ya usimamizi wa Sheria lakini pia Chama kinaweza kupata ushauri wa busara na njia mbadala kutoka Ofisi ya Mrasis kabla ya kufuta mikopo vitabuni

#### **1.20 Ufutiliaji Mkopo Baada Ya Kufutwa Vitabuni**

Zoezi la kufuta mikopo si sababu ya kumsamche mkopaji wala Bodi kubweteka, la hasha! Hii ni taratibu za kiuhasibu tu kusafisha vitabu na hivyo mwanachama lazima aendelee kutafutwa na kudaiwa mkopo husika kwa mbinu na namna yeoyote ile. Endapo atarejesha, sedha hizo zitaingizwa kwenye mapato ya Chama kama Mapato yatokanayo na Mikopo iliyofutwa.

#### **1.21 Uhuishaji wa Sera**

Sera hii itafanyiwa mapitio kila mwaka na inaweza kuhuishwa mara moja ndani ya mwaka ama kulingana na mahitaji na inapostahili.

## 1.22 Uidhinishwaji wa Sera

Sera hii imetayarishwa na kupitishwa Bodi ya UDOM SACCOS Ltd kwa niaba ya wanachama; katika kikao kilichofanyika tarehe 05.... Mwezi 04..., mwaka 2020..... Na itaanza kutumika tarehe 05..., mwezi 08, mwaka 2020 baada ya kuidhinishwa na Mrasis.

  
Mrasis wa Vyama yya Ushirika  
Tarehe 05/08/2020

